

TANGAZO LA SERIKALI NA. 817 la tarehe 20 Septemba 2024

SHERIA YA UNUNUZI WA UMMA,
(SURA YA 410)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 129)

**KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UNUNUZI WA
UMMA ZA MWAKA 2024**

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Ununuzi wa Umma, ambazo hapa zimerejewa kama “Kanuni kuu”.

Marekebisho
ya kanuni ya
167

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 167-
(a) kwa kufuta maneno “milioni mia moja” katika kanuni ndogo ya (2) na badala yake kuweka maneno “milioni mia tano”;
(b) kwa kuongeza baada ya kanuni ndogo ya (2) kanuni ndogo ifuatayo:

“(3) Bila kujali kanuni ndogo ya (2), pale ambapo kuna manufaa ya umma na gharama ya kufanya kazi za ujenzi kwa kutumia rasilimali za ndani inakadiriwa kuwa zaidi ya shilingi milioni mia tano, afisa masuuli atapaswa kutoa idhini ya kutumika kwa utaratibu huo baada ya

- (a) kutathmini hitaji la utekelezaji wa kazi za ujenzi husika kwa kutumia rasilimali za ndani;
- (b) kuhakikisha uwepo wa watumishi wa umma wenye sifa za kusimamia ujenzi husika kwa mujibu wa mwongozo utakaotolewa na Mamlaka;
- (c) kuhakikisha uwepo wa mafundi wenye sifa stahiki kwa kuzingatia aina ya kazi ya ujenzi katika mradi husika; na
- (d) kufanya tathmini ya gharama na

Tangazo la Serikali Na. 817(Linaendelea)

muda wa utekelezaji wa mradi kwa kutumia rasilimali za ndani ikilinganishwa na matumizi ya njia zingine za utekelezaji wa kazi za ujenzi.”;

- (c) katika kanuni ndogo ya (4), kwa kufuta rejea ya “kanuni ya ndogo ya (3)(b)” na badala yake kuweka rejea ya “kanuni ndogo ya (4)(b)”;
- (d) katika kanuni ndogo ya (7), kwa kufuta rejea ya “kanuni ya ndogo ya (6)” na badala yake kuweka rejea ya “kanuni ndogo ya (7)”;
- (e) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo ya (3) hadi (9) kuwa kanuni ndogo ya 4 hadi 10, mtawalia.”.

Kuongezwa
kwa kanuni ya
167A

3. Kanuni kuu zinarekebisha kwa kuongeza mara baada ya kanuni ya 167 kanuni ifuatayo:

“Wajibu wa
afisa
masuuli na
Mamlaka
katika
matumizi ya
rasilimali za
ndani

167A.-(1) Afisa masuuli atahakikisha kuwa anawasilisha kwa Mamlaka-

- (a) taarifa ya kuanza kazi za ujenzi kwa kutumia rasilimali za ndani ndani ya siku saba baada ya kuanza ujenzi; na
- (b) taarifa za utekelezaji wa kazi za ujenzi uliokwishakamilika kwa kila awamu ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kukamilika kwa kazi za ujenzi husika.

(2) Endapo kazi za ujenzi zimetokelezwa kama Mamlaka ilivyotaarifiwa chini ya kanuni ndogo ya (1), Mamlaka itafanya ukaguzi maalum wa thamani ya fedha ili kujiridhisha kuhusu hitaji la matumizi ya rasilimali za ndani katika kazi za ujenzi husika, thamani halisi ya fedha ya bidhaa na huduma zilizotumika na muda wa ujenzi husika.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo

Tangazo la Serikali Na. 817(Linaendelea)

ya (2), iwapo baada ya ukaguzi Mamlaka itabaini kuwa taratibu za utekelezaji wa masharti ya matumizi ya rasilimali za ndani zimekiukwa na taasisi nunuzi, Mamlaka itapendekeza kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali au chombo kingine chenye mamlaka hatua stahiki za kuchukuliwa dhidi ya afisa masuuli wa taasisi nunuzi husika.”.

Dodoma,
18 Septemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
Waziri wa Fedha